**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**

---

**Kumb: Na. AB.113/388/01/67** **Tarehe: 05 Januari, 2024**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA DEREVA WA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo anakaribisha maombi ya kazi ya udereva wa mkataba kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi kumi na nne (14) kama ilivyoainishwa katika tangazo hili.

### 1.0 DEREVA NAFASI 14.

### 1.1 SIFA ZA MUOMBAJI

- ✓ Awe na cheti cha kidato cha Nne (IV).
- ✓ Leseni ya Daraja la C au E ya uendeshaji Magari ambayo imefanyiwa kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila ya kusababisha ajali.
- ✓ Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi stadi (VETA), NIT au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.2 MAJUKUMU YA KAZI

- ✓ Kukagúa gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ✓ Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- ✓ Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- ✓ Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- ✓ Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- ✓ Kufanya usafi wa gari

### 1.3 MSHAHARA

- ✓ Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa atalipwa mshahara wa Shilingi laki tatu (300,000) kwa mwezi.

**1.4 MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18 - 45.

ii. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.

iii. Barua ya muombaji ioneshe anuani anayotumia kwa sasa pamoja na namba za simu ikiambatana na:-

   a) Nakala za vyeti vya taaluma.

   b) Nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

   c) Maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

   d) Picha mbili (2) za "Passport Size" za hivi karibuni.

   e) Kitambulisho au namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA)

iv. Waombaji wote waliowahi kupatikana na kosa la jinai hatafikiriwa

v. "Testmonial", "Provisional Results", Statement of result", hati za matokeo ya kidato cha nne (FORM IV RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.

iv. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

Waombaji wenye sifa wanatakiwa kutuma maombi kupitia Posta kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi wa Manispaa,**
**Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo,**
**S.L.P 55068.**
**DAR ES SALAAM.**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 19 Januari, 2024 Saa 9:30 Alasiri**

**NB: Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri www.ubungomc.go.tz**

Elias R. Nyiruhungwa
**MKURUGENZI WA MANISPAA**